

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAA

NYIHARA SEKONDARI
S. L.P 1377
MUSOMA
30/11/2023

KUMB NA. NYHRSS/JOIN/F 1/ 2024

MWANAFUNZI

YAH; KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA KUTWA YA NYIHARA
SEKONDARI KWA MWAKA WA MASOMO 2024

Tafadhari rejea mada tajwa hapo juu. Napenda kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na shule yetu ya Nyihara sekondari kwa mwaka wa masomo 2024. Shule inapatikana tarafa ya Suba, kata ya Kyang'ombe, kijiji cha Nyihara. Hivyo kwa barua hii unapaswa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 8/1/2024(siku ya kufungua shule), mwisho wa kuripoti ni tarehe 19/1/2024 siku ya ijumaa. Hata hivyo mahitaji ni kama ifuatavyo ;-

1. SARE ZA SHULE

- ❖ Shati mbili nyeupe(Tomato) za mikono mifupi kwa wasichana na wavulana
- ❖ Tai mbili, damu yam zee na kijivu
- ❖ Suruali mbili, kijivu na damu yam zee zenye marinda kiunoni , turnup na isiwe ya kubana kwa wavulana
- ❖ Wasichana Sketi mbili, damu ya mzee na kijivu zenye urefu unaofika miguuni kwa kutumia vitambaa vizito visivyoonesha maumbo ya ndani.
- ❖ Soksi jozi mbili, wasichana nyeupe na wavulana nyeusi
- ❖ Viatu vyeusi jozi mbili vya Kamba visivyo na kisigino kirefu wala kuchongoka mbele
- ❖ T- sheti moja ya bluu yenye kora
- ❖ Vifaa nya michezo (trakisuti jozi moja nyeusi yenye misitari nyeupe pembeni, raba za michezo na soksi)

2. VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA MAHITAJI MUHIMU

- ❖ Kaunta 9 kuanzia quire two za kuandikia nukuu, daftari ndogo 9 kwaajili ya majaribio pamoja na English course, kalamu za wino na zamkaa kwaajili ya kuandikia na kuchorea
- ❖ Kamusi ya kingereza
- ❖ Mathematical set kujifunzia somo la hisabati
- ❖ **Bando moja ya lim paper** kwaajili ya mitihani na mazoezi mbalimbali
- ❖ Chakula (mahindi amboni 2, maharage kilo 2 pamoja na pesa Tsh 8000/=)
- ❖ Kiti na meza yenye uvungu kwaajili kujifunzia

3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia namba 10 ya mwaka 1995. Aidha kwa kuzingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Raisi TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Hivyo ukiwa kama mwanafunzi wa shule hii unatakiwa kufuata maelekezo yafuatayo;-

- I. Kuripoti shule muda wa saa 1:00 asubuhi kila siku za masomo
- II. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
- III. Kuheshimu viongozi, walimu wafanyakazi wengine, wazazi, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla
- IV. Kushiriki shughuli mbalimbali za shule, ikiwa pamoja za zile utakazopangiwa na walimu pamoja na viongozi wako
- V. Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule
- VI. Kizingatia ratiba ya shule kama inavyoelekeza
- VII. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifumaelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote uwapo shuleni
- VIII. Hauruhusiwi kuwa na simu katika eneo la shule
- IX. Kutunza mali ya umma

MUHIMU: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;

- i. Wizi
- ii. Ubakaji au kumpa mimba msichana
- iii. Kipiga au kupigana
- iv. Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kutoa mimba
- v. Uasherati na ushoga
- vi. Kukataa adhabu kwa makusudi
- vii. Kudharau bendera ya taifa
- viii. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- ix. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama bangi, mirungi, sigara na kuberi
- x. Kugoma, kuchochea, kuongoza na kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu

TANBIHI: hakikisha siku ya kwanza unaporipoti shule ufike na **Medical Examination form** ambayo imejazwa na **mganga mkuu wa hospitali ya serikali na si vinginenyo.**

Hongera sana,

.....

VICTOR PAUL KIHAGA

(MKUU WA SHULE) SIMU; 0717 997 639